WAJIBU WA TAASISI NA VIONGOZI WA DINI
KATIKAKUHUDUMIA WAGONJWA
NA
SK. ABDULLA TALIB ABDULLA

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambae kwa uwezo ameumba siha na maradhi ili atujaribu. Sala na salamu zimshukie Mtume SAW alietuhimiza sana kujikinga, kujitibu, na kuwahudumia wagonjwa nae akawa mfano mwema wa yote aliyoyahimiza. Mwenyezi Mungu amrehemu pamoja na jamaa zake, wafuasi wake na wale wote wanaofuata mwenendo wake wa kutunza afya, kukinga maradhi na kutibu. Ama baada ya hayo.

Kila mtu anaweza kuugua au kuuguliwa na maradhi ya muda mrefu au ya muda mfupi. Aidha anaweza kuuguwa maradhi yanayotibika au ambayo bado tiba yake haijagundulika. Maradhi hayo yanaweza kumzuwia kufanya shughuli zake zote au akaweza kuzifanya baadhi lakini sio kwa ufanisi. Kwa maana hiyo amesema Mtume SAW ***" Yatumieni vyema mambo matano kabla ya matano..."*** na akataja katika mambo hayo ***" na siha yako kabla ya maradhi yako".***

Ulimwengu kwa kufahamu hilo umekuwa ukianzisha kampeni mbali mbali dhidi ya maradhi ambayo yamekuwa yakiathiri sana wanadamu na hata wanyama. Maradhi kama vile kifua kikuu, Ukimwi, malaria, kipindupindu na mengineyo mengi yamepewa kipaumbele katika kukabiliana nayo hapa kwetu Zanzibar. Hivyo viongozi na wafuasi wa uislamu hanta budi kuunga mkono juhudi hizi kwani zinaendana na makusudio ya sheria ya kiislamu.

Tunapozungumza viongozi wa dini, tunakusudia viongozi wote wa dini katika ngazi zote. Wanaingia viongozi wa ngazi za juu kama Khalifa, Mufti na wanaingia mpaka Sheikh wa Mtaa, Mwalimu wa Madrasa, Imamu au hata mlinganiaji. Kwani amesema Mtume S.A.W ***"Nyote ni wachunga na nyote mtaulizwa kuhusiana na kile mnachokichunga".*** Hivyo kila mmoja ana wajibu na dhamana katika lile eneo ambalo ana mamlaka nalo na kwa vile Mtume alishughulikia afya ya kiroho na afya ya kiwiliwili na viongozi wa kidini ndio warithi wa Mtume basi na wao hawana budi kushughulikia yote mawili..

Ama taasisi ya kidini ni kikundi chochote au mjumuiko wowote wa watu ambao umeundwa kidini kwa lengo mahsusi linaloridhiwa na Allah. Taasisi hii inaweza kuwa familia, Jumiya, Msikiti, Chuo, Madrasa n.k. Mwenyezi Mungu amezitaja baadhi ya taasisi za kidini ambazo ni nyumba za ibada aliposema. ***((Na kama Mwenyezi Mungu asingaliwakinga watu, baadhi yao kwa wengine bila ya shaka yangalivunjwa Mahekalu na Makanisa na nyumba za ibada na Misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi)) 22:40.*** Kwa vile dini inapanga mahusiano baina ya mtu na Mola wake na baina ya mja na mja mwengine.

Taasisi na viongozi wa dini wana wajibu wa kusimamia afya za watu hasa pale wanapohisi kuwa waumini wanakabiliwa na tishio la maradhi fulani ni lazima zichukuliwe hatua mahsusi.

USHAURI NASAHA

Dini imehimiza sana mambo yanayohusu ushauri na kutoa nasaha. Mwenyezi Mungu amewasifu Waislamu aliposema. ***"Na mambo yao huenda kwa kushauriana baina yao"(42:38)*** na akamuamrisha Mtume S.A.W kwa kusema ***"Na washauri katika mambo"(3:159).*** Na akawataka waumini wasaidiana katika mambo mema na ucha Mungu ikiwemo kupeana nasaha na ushauri kama alivyosema ***"Na saidianeni katika wema na ucha Mungu"(5:2).*** Na Mtume S.A.W akasisitiza umuhimu wa kunasihiana aliposema ***"Dini ni nasaha".*** Hivyo ni vyema tukatumia wakati huu kujielimisha na kuwaelimisha wafuasi wetu ili waweze kujikinga Marathi thakili yakiwemo ya kifua kikuu na ukimwi. Tutambue kuwa kupeana nasaha katika afya ya kiwiliwili ni jambo muhimu mno katika wakati huu ili waumini wawe wenye nguvu ambao ndio bora na wanaopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu.Mafunzo ya dini hulifanya jambo lisilowezekana kuwa, na humbadilisha mtu kwa namna isiyotarajiwa.

Ushauri nasaha ni njia ya kujenga uhusiano baina ya mtu anaepewa huo ushauri na mtoaji ushauri ili kusaidia mpewaji huyo kutafuta njia nzuri ya kuondosha tatizo linalomkabili. Ni njia ya mazungumzo ambayo yanahitaji utulivu, busara na hekima ili upate kumuongoza vyema yule unayemkusudia ili atoe haki au njia sadidi mwenyewe kama alivyosema Imam Shafii (Rahimahullah) ***"Mimi hupenda ninapozungumza na mtu(suluhisho) haki aitamke mwenyewe".***

KUHUDUMIA WAGONJWA MAJUMBANI

Mtume SAW alikuwa na tabia ya kuwazuru wagonjwa na akasisitiza sana wafuasi wake kulifanya hilo. Katika siku hizi huduma nyingi za kiafya hutolewa hospitali na madaktari na waguuzi lakini bado waislamu wanayonafasi ya kusaidia huduma hizo kwa kutoa michango mbali mbali, kusaidia usafi na hata kuwafariji wagonjwa nakuwaombea dua.

Kuna kundi la pili la wagonjwa ambalo kikweli limesahauliwa na wengi. Hili nilile linalougulia majumbani namara nyingi uwa ni wagonjwa wa maradhi ya muda mrefu. Kuhudumia wagonjwa majumbani ni huduma yoyote ya kiafya au kijamii itolewayo kwa mgonjwa mwenye maradhi ya muda mrefu (ukiwemo UKIMWI) majumbani wao. Huduma hizi husaidia kushibisha mahitaji ya mgonjwa na kutoa fursa kwa kumuelimisha yeye na waliomzunguka, pia kutoa ushauri nasaha.

Tunapoangalia mafunzo ya dini zetu yanatuhimizi sana kuwakagua wagonjwa wajumbani ili kuwasaidia na kuwapa ushauri nasaha. Miongoni mwa hekma kubwa za Waislamu kuwekewa Sala tano ni kukutana na kujuana.

Waislamu wa awali walikuwa na kawaida kama Muislamu asipohudhuria msikiti wengi wao huenda kumkagua kwa kukhofia kuwa asije akawa mgonjwa au mwenye dharura kubwa kwani kama alivyosema Mtume S.A.W ***((Hawi mwenye kuamini mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake yale anayojipendelea nafsi yake)).***

Hebu tumuangalie Mtume S.A.W alipokuwa hakumuona Sahaba wake aitwae Thauban, aliuliza na akaambiwa yu mgojwa kitandani. Hapo hapo akatoka kwenda kumkagua, akamsikiliza shida yake na kumpa nasaha ambazo ni funzo kubwa kwetu na zilimaliza kabisa kabisa tatizo lake. Sio kila ugonjwa unatibika kwa dawa za kula au kunywa tu bali yako mengi ambayo yanawasumbua wagonjwa na iwapo yatapatiwa maneno mazuri au mafahamiano ya kiroho basi tatizo litaondoka na wagonjwa wataishi kwa matumaini. Mtume SAW alisema : ***"Tambua ewe Thauban kuwa hakika mja hufufuliwa pamoja na wale anaowapenda."***

Ikiwa sheria ya Kiislamu inaamrisha mtu aliekwisha kuhukumiwa kifo atembelewe mara kwa mara na watu wenye elimu na hekma ili wampe mawaidha, kumnasihi na kumshauri; jee mtu mgonjwa ambae ugonjwa wake ni wa muda mrefu na wenye matatizo mengi hukumu yake itakuwaje?

Dini imebainisha adabu nyingi ambazo inatupasa tushikamane nazo ikiwemo kuwahudumia wagonjwa,kuwasaidia, kuwaombea dua wapone, kuwausia subira na uvumilivu, kuwasemesha maneno mazuri ambayo yatawapa matumaini na kuipa nguvu roho yao na kuwatimizia hali zao. Pia kumetajwa fadhila nyingi anazozipata mgonjwa na yule anaemkaguwa ambazo zinahitaji kukumbushwa. Amepokea Bukhari kuwa amesema Mtume S.A.W ***"Mlishe mwenye njaa, mkague mgojwa na mfungue mfungwa"***. Imepokewa na Bukhari na Muslim kuwa amesema Mtume S.A.W ***"Haki za Muislamu kwa Muislamu mwengine ni sita…akikutaka nasaha basi umnasihi, anapokuwa mgonjwa umkague na akifa ushindikize jeneza lake".***

Katika hadithil qudusi iliyopokewa na Muslim inasimuliwa kuwa Mtume S.A.W amesema "***Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema siku ya Kiama: Ewe mwanadamu nimeumwa na hukuja kunikagua". Atajibu ewe Mola, vipi nikukague nawe ndio Mola wa Walimwengu wote? Atasema "Hukujua kwamba Mja wangu fulani ameumwa nawe hukumkagua, jee hukuwa ukitambua kwamba lau kama ungemkagua ungelinikuta kwake? Ewe mwanadamu nimekutaka unilishe nawe hukunilisha" Atajibu ewe Mola vipi nikulishe nawe ndie Mola wa Walimwengu wote. Atasema "Hukumbuki kwamba amekutaka chakula mja wangu fulani nawe hukumlisha. Jee hukuwa ukitambua lau kama ungelimlisha ungelikikuta kwangu?…"***

Hapana ubaya kumkagua mgojwa alie na jinsia nyengine kama ilivyopokewa na Imam Bukhari kuwa Umu Dardai alimkagua mwanamme wa Kiansari katika ahlu Masjid na ikapokewa kuwa bibi Aisha alikwenda kumkagua baba yake na Bilal.

Aidha hapana ubaya wa kukagua mtu wa itikadi au dini nyengineyo kama ilivyopokewa kuwa Mtume S.A.W alikwenda kumkagua kijana wa Kiyahudi na alikuwa akimkagua na kumsaidia Ami yake Abu Talib hali ya kuwa ni mshirikina.

WAJIBU WA TAASISI NA VIONGOZI WA DINI

Ni vyema kwa taasisi na viongozi wa dini tukajiuliza masuala yafuatayo ili tuweze kujihesabu wenyewe kabla haijafika siku ya kuhesabiwa:-

- Jee Wagonjwa walio majumbani na familia zao wanayo mahitaji ambayo yanahitaji kushibishwa na asasi na viongozi wa dini au hawana?
- Ni mikakati gani mahsusi tuliyojipangia kwa watu hao au Mwenyezi Mungu hatotuuliza na jamii haitotuhesabu? Amesema mtukufu **"Kisha mtaulizwa siku hiyo kuhusiana na neema"**
- Jee hakuna wagonjwa waliotengwa, wanaosimbuliwa na kusimangwa, wanaodhulumiwa n.k. kiasi cha kukata tamaa wao au wao na familia zao?Nini wajibu wetu katika kutatua hayo au hayatuhusu?
- Haki za wazee, watoto, jamaa, majirani na udugu wa kidini zinakoma kwa kuuguwa na kuuguliwa ama zinaendelea? Taaluma hii inahtiaji kutolewa na Madaktari, waganga wa kienyeji au nani? Jee asasi na viongozi wa dini haiwahusu?
- Kitu ambacho hakiwezi kukamilika wajibu ila kwacho, nacho huwa ni wajibu. Hali ilivyofikia sasa kuhusu maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kifua kikuu; namna bora ya kuwahudumia wagonjwa bila ya kuambukizwa n.k. Jee kutokujifunza elimu ya msingi ya UKIMWI na kifua kikuu kutakuwa na hukmu gani?
- Jee dini yetu inatuelekeza nini kuhusu kutoa ushauri nasaha hasa kwa watu wenye matatizo kama wagonjwa, wanaouguliwa au hata walioteleza kwa kuwaacha wagonjwa wao? Au haina mafunzo yoyote? Mafundisho hayo, miongozo hiyo, nasaha hizo za kidini inatakiwa zitolewe na nani?
- Jee hatuna jukumu au mchango wowote wa kushibisha au kusaidia mgonjwa katika mahitaji yake ya kimwili, kiafya, kitiba,kilishe, kiroho, kiusafi, kisaikolojia.

Ni matumaini yangu kuwa tukiyajibu maswali haya kwa ikhlasi na ukweli tutajuwa wajibu wetu kama viongozi wa dini aidha wajibu wa taasisi zetu katika kutoa ushauri nasaha na kuwahudhumia wagonjwa majumbani.

Ninamuomba Allah atuwafikishe katika haki na yale anayoyaridhia.

Wabillah tawfiq